# Yakobo

*Salamu*

1 Yakobo, mtumwa wa Mungu na wa Bwana
Isa Al-Masihi.

Kwa makabila kumi na mawili yaliyotawanyika ulimwenguni.

Salamu.

*Imani na hekima*

2 Ndugu zangu, hesabuni kuwa ni furaha tupu
mnapopatwa na majaribu mbalimbali,
3 kwa sababu mnajua ya kuwa kujaribiwa kwa
imani yenu huleta saburi.
4 Acheni saburi ikamilishe kazi yake, ili mpate
kuwa wakamilifu na watimilifu, bila kupun-
gukiwa chochote.
5 Kama mtu yeyote miongoni mwenu amepun-
gukiwa na hekima, basi amwombe Mungu, yeye
awapaye watu wote kwa ukarimu wala hana
kinyongo, naye atapewa.
6 Lakini anapoomba, lazima aamini wala asiwe
na shaka, kwa sababu mtu aliye na shaka ni
kama wimbi la bahari, linalopeperushwa na up-
epo na kutupwa huku na huko.
7 Mtu kama huyo asidhani ya kuwa atapata kitu
chochote kutoka kwa Bwana Isa.
8 Yeye ni mtu mwenye nia mbili, mwenye
kusitasita katika njia zake zote.

*Umaskini na utajiri*

9 Ndugu asiye na cheo kikubwa yampasa ajivu-
nie hali hiyo maana ametukuzwa.
10 Lakini yeye aliye tajiri afurahi kwa kuwa
ameshushwa, kwa sababu atatoweka kama ua la
shambani.
11 Kwa maana jua kali huchomoza na
kuyakausha majani ya mmea, nalo ua lake
linaanguka, na uzuri wake unaharibika. Vivyo
hivyo tajiri naye atanyauka akiwa anaendelea
na shughuli zake.

### *Kujaribiwa*

12 Heri mtu anayevumilia wakati wa majaribu,
kwa sababu akiisha kushinda hilo jaribio at-
apewa taji lile la uzima Mungu alilowaahidia
wale wanaompenda.
13 Mtu anapojaribiwa asiseme, "Ninajaribiwa
na Mungu." Kwa maana Mungu hawezi ku-
jaribiwa na maovu wala yeye hamjaribu mtu
yeyote.
14 Lakini kila mtu hujaribiwa wakati
anapovutwa na kudanganywa na tamaa zake
mwenyewe zilizo mbaya.
15 Basi ile tamaa mbaya ikishachukua mimba
huzaa dhambi, nayo ile dhambi ikikomaa huzaa
mauti.
16 Ndugu zangu wapendwa, msidanganyike.
17 Kila kitolewacho kilicho chema na kilicho
kamili hutoka juu, na hushuka kutoka kwa Baba
wa mianga, ambaye kwake hakuna kubadilika,
wala kivuli cha kugeukageuka.
18 Kwa mapenzi yake mwenyewe alituzaa kwa
neno la kweli, kusudi tuwe kama mazao ya
kwanza katika viumbe vyake vyote.

### *Kusikia na kutenda*

19 Ndugu zangu wapendwa, fahamuni jambo
hili: Kila mtu awe mwepesi wa kusikiliza, lakini
asiwe mwepesi wa kusema wala wa kukasirika.
20 Kwa maana hasira ya mwanadamu haitendi
haki ya Mungu.
21 Kwa hiyo, ondoleeni mbali uchafu wote na
uovu ambao umezidi kuwa mwingi, mkalipokee
kwa unyenyekevu lile Neno lililopandwa ndani
yenu ambalo laweza kuokoa nafsi zenu.

22 Basi kuweni watendaji wa Neno, wala msiwe
wasikiaji tu, huku mkijidanganya nafsi zenu.
23 Kwa maana kama mtu ni msikiaji tu wa Neno
wala hatendi kile linachosema, yeye ni kama mtu
ajitazamaye uso wake kwenye kioo
24 na baada ya kujiona alivyo, huenda zake na
husahau upesi jinsi alivyo.
25 Lakini yeye anayeangalia kwa makini katika
sheria kamilifu iletayo uhuru, naye akaende-
lea kufanya hivyo bila kusahau, bali akatenda
alichosikia, basi atabarikiwa katika kile ana-
chofanya.

26 Kama mtu akidhani ya kuwa anayo dini
lakini hauzuii ulimi wake kwa hatamu, hujidan-
ganya moyoni mwake, wala dini yake haifai kitu.
27 Dini iliyo safi, isiyo na uchafu, inayokubalika
mbele za Mungu, Baba* yetu, ndiyo hii: ni
kuwasaidia yatima na wajane katika dhiki zao na
kujilinda usitiwe madoa na dunia.

* **1:27** Kwa mwanadamu, Mwenyezi Mungu ni Baba kupitia uhusiano unaopatikana katika kumtumaini Isa Al-Masihi.

# 2

### *Onyo kuhusu upendeleo*

1 Ndugu zangu, waumini katika imani ya
Bwana wetu wa utukufu, Isa Al-Masihi, hawa-
paswi kuwa na upendeleo.
2 Je, ikiwa mtu anakuja katika kusanyiko
lenu akiwa amevaa pete ya dhahabu na mavazi
mazuri, na kisha akaingia mtu maskini aliyevaa
mavazi yaliyochakaa.
3 Mkimpa heshima yule aliyevaa mavazi
mazuri na kumwambia, “Keti hapa mahali
pazuri,” lakini yule maskini mkamwambia,
“Wewe simama pale,” au “Keti hapa sakafuni
karibu na miguu yangu,”
4 je, hamjabagua kati yenu wenyewe na kuwa
mahakimu wenye mawazo maovu?

5 Ndugu zangu, sikilizeni: Je, si Mungu huwach-
agua wale walio maskini machoni pa ulimwengu
kuwa matajiri katika imani na kuurithi ufalme
aliowaahidi wale wanaompenda?
6 Lakini ninyi mmemdharau yule aliye mask-
ini. Je, hao matajiri si ndio wanaowadhulumu na
kuwaburuta mahakamani?
7 Je, si wao wanalikufuru jina lile bora sana
mliloitiwa?
8 Kama kweli mnaitimiza ile sheria ya ki-
falme inayopatikana katika Maandiko, isemayo,
“Mpende jirani yako kama unavyoipenda nafsi
yako,” mnafanya vyema.
9 Lakini mkiwapendelea watu, mnatenda
dhambi, na sheria inawahukumu kuwa wakosaji.

10 Kwa maana mtu yeyote anayeishika sheria
yote lakini akajikwaa katika kipengele kimoja tu,
ana hatia ya kuivunja sheria yote.
11 Kwa sababu yeye aliyesema, “Usizini,”
alisema pia, “Usiue.” Basi kama huzini lakini
unaua, umekuwa mvunjaji wa sheria.
12 Hivyo semeni na kutenda kama watu
watakaohukumiwa kwa sheria ile iletayo uhuru.
13 Kwa kuwa hukumu bila huruma itatolewa
kwa mtu yeyote asiyekuwa na huruma. Huruma
huishinda hukumu.

### *Imani na matendo*

14 Ndugu zangu, yafaa nini ikiwa mtu atadai
kuwa anayo imani lakini hana matendo? Je,
imani kama hiyo yaweza kumwokoa?
15 Ikiwa ndugu yako au dada hana mavazi wala
chakula,
16 naye mmoja wenu akamwambia, “Nenda
zako kwa amani, ukaote moto na kushiba,”
pasipo kumpatia yale mahitaji ya mwili aliyop-
ungukiwa, yafaa nini?
17 Vivyo hivyo, imani peke yake, kama
haikuambatana na matendo, imekufa.
18 Lakini mtu mwingine atasema, “Wewe unayo
imani; mimi ninayo matendo.”

Nioneshe imani yako pasipo matendo nami
nitakuonesha imani yangu kwa matendo.
19 Unaamini kwamba kuna Mungu mmoja.
Vyema! Hata mashetani wanaamini hivyo na
kutetemeka.
20 Ewe mpumbavu! Je, wataka kujua kwamba
imani bila matendo haifai kitu?

21 Je, Ibrahimu baba yetu hakuhesabiwa haki
kwa kile alichotenda, alipomtoa mwanawe Isaka
madhabahuni?
22 Unaona jinsi imani yake na matendo yake
vilikuwa vinatenda kazi pamoja, nayo imani
yake ikakamilishwa na kile alichotenda.
23 Kwa njia hiyo likatimizwa andiko lisemalo,
"Ibrahimu alimwamini Mungu, na ikahesabiwa
kwake kuwa haki," naye akaitwa rafiki wa
Mungu.
24 Mnaona kwamba mtu huhesabiwa haki kwa
yale anayotenda wala si kwa imani peke yake.
25 Vivyo hivyo, hata Rahabu, yule kahaba:
je, hakuhesabiwa haki kwa yale aliyotenda
alipowapokea wale wapelelezi na kuwaambia
waende njia nyingine?
26 Kama vile mwili pasipo roho umekufa, kad-
halika nayo imani pasipo matendo imekufa.

# 3

### *Kuufuga ulimi*

1 Ndugu zangu, msiwe walimu wengi, kwa
maana mnafahamu kwamba sisi tufundishao tu-
tahukumiwa vikali zaidi.
2 Sisi sote tunajikwaa katika mambo mengi.
Ikiwa mtu yeyote hakosei kamwe katika yale
anayosema, yeye ni mkamilifu, naye anaweza
kuuzuia pia na mwili wake wote.
3 Tunapotia lijamu kwenye vinywa vya farasi ili
kuwafanya watutii, tunaweza kuigeuza miili yao
yote.
4 Au chukua mfano wa meli: ingawa ni
kubwa sana, nazo hupelekwa na upepo mkali,

zinaelekezwa kwa usukani mdogo sana kokote wanakotaka nahodha.
5 Vivyo hivyo ulimi ni kiungo kidogo
sana katika mwili, lakini hujivuna majivuno makuu. Fikirini jinsi moto mdogo unavyoweza kuteketeza msitu mkubwa!
6 Ulimi pia ni moto, ndio ulimwengu wa
uovu kati ya viungo vya mwili. Ulimi huutia mwili wote wa mtu unajisi na kuuwasha moto mfumo mzima wa maisha yake, nao wenyewe huchomwa moto wa Jehanamu.

7 Kwa maana kila aina ya wanyama, ndege,
wanyama watambaao na viumbe vya baharini hufugika na hufugwa na binadamu,
8 lakini hakuna mtu awezaye kuufuga ulimi. Ni
uovu usiotulia, umejaa sumu iletayo mauti.

9 Kwa ulimi tunamhimidi Mwenyezi Mungu
na Baba* yetu, na kwa huo twawalaani watu walioumbwa kwa mfano wa Mungu.
10 Katika kinywa kile kile hutoka baraka na
laana. Ndugu zangu, haistahili kuwa hivyo.
11 Je, chemchemi moja inaweza kutoa katika
tundu moja maji matamu na maji ya chumvi?
12 Je, ndugu zangu, mtini unaweza kuzaa
zeituni, au mzabibu kuzaa tini? Wala chemchemi ya maji ya chumvi haiwezi kutoa maji matamu.

### *Aina mbili za hekima*

13 Ni nani aliye na hekima na ufahamu mion-
goni mwenu? Basi na aioneshe hiyo kwa maisha

---

* **3:9** Kwa mwanadamu, Mwenyezi Mungu ni Baba kupitia uhusiano unaopatikana katika kumtumaini Isa Al-Masihi.

yake mema na kwa matendo yake yaliyotendwa
kwa unyenyekevu utokanao na hekima.
14 Lakini ikiwa mna wivu na ni wenye chuki
na ugomvi mioyoni mwenu, msijisifu kwa ajili ya
hayo wala msiikatae kweli.
15 Hekima kama hiyo haishuki kutoka mbin-
guni, bali ni ya kidunia, isiyo ya kiroho, na ya
kishetani.
16 Kwa maana panapokuwa na wivu na ubi-
nafsi, ndipo penye machafuko na uovu wa kila
namna.
17 Lakini hekima inayotoka mbinguni kwanza
ni safi, kisha inapenda amani, tena ni ya upole,
iliyo tayari kusikiliza wengine kwa unyenyekevu,
iliyojaa huruma na matunda mema, isiyopende-
lea mtu, tena isiyokuwa na unafiki.
18 Mavuno ya haki hupandwa katika amani na
wale wafanyao amani.

# 4

*Jinyenyekezeni kwa Mwenyezi Mungu*

1 Ni kitu gani kinachosababisha mapigano na
ugomvi miongoni mwenu? Je, haya hayatokani
na tamaa zenu zinazoshindana ndani yenu?
2 Mnatamani lakini hampati, kwa hiyo mwaua.
Mwatamani kupata lakini hampati vile mnavy-
otaka, kwa hiyo mnajitia katika magomvi na
mapigano. Mmepungukiwa kwa sababu hamm-
wombi Mungu.
3 Mnapoomba hampati kwa sababu mnaomba
kwa nia mbaya, ili mpate kuvitumia hivyo
mtakavyopata kwa tamaa zenu.

4 Ninyi wanaume na wanawake wazinzi, hamjui kwamba urafiki na dunia ni uadui na Mungu? Kwa hiyo mtu yeyote anayetaka kuwa rafiki wa dunia hufanyika adui wa Mungu.
5 Au mwadhani kwamba Maandiko yasema bure kuwa huyo Roho ambaye Mungu amemweka ndani yetu hututamani kiasi cha kuona wivu?
6 Lakini yeye hutupatia neema zaidi. Hii ndiyo sababu Maandiko yasema:
“Mungu huwapinga wenye kiburi,
lakini huwapa wanyenyekevu neema.”
7 Basi mtiini Mungu. Mpingeni ibilisi, naye atawakimbia.
8 Mkaribieni Mungu, naye atawakaribia. Itakaseni mikono yenu ninyi wenye dhambi, na kuisafisha mioyo yenu ninyi wenye nia mbili.
9 Huzunikeni, na mwomboleze, na kulia. Kicheko chenu na kigeuzwe kuwa kuomboleza, na furaha yenu kuwa huzuni.
10 Jinyenyekezeni mbele za Mwenyezi Mungu, naye atawainua.

### *Onyo kuhusu kuwahukumu wengine*

11 Ndugu, msineneane mabaya ninyi kwa ninyi. Mtu yeyote anayesema mabaya dhidi ya ndugu yake au kumhukumu, anasema dhidi ya sheria na kuihukumu. Unapoihukumu sheria, basi huishiki sheria, bali umekuwa hakimu wa kuihukumu hiyo sheria.
12 Yuko Mtoa sheria mmoja tu na yeye peke yake ndiye Hakimu; ndiye awezaye kuokoa au kuangamiza. Lakini wewe ni nani hata umhukumu jirani yako?

*Kujivuna kwa ajili ya kesho*

13 Basi sikilizeni ninyi msemao, “Leo au kesho
tutaenda katika mji huu ama ule tukae humo
mwaka mmoja, tufanye biashara na kupata
faida.”
14 Lakini hamjui hata litakalotukia kesho.
Maisha yenu ni nini? Ninyi ni ukungu ambao
huonekana kwa kitambo kidogo kisha hutoweka.
15 Badala yake, inawapasa kusema, “Kama
Mwenyezi Mungu akipenda, tutaishi na kufanya
hili ama lile.”
16 Ilivyo sasa, mnajisifu na kujigamba. Kujisifu
kote kwa namna hii ni uovu.
17 Basi mtu yeyote anayejua jema limpasalo
kutenda, lakini asilitende, mtu huyo anatenda
dhambi.

# 5

*Onyo kwa matajiri*

1 Basi sikilizeni, ninyi matajiri, lieni na kuom-
boleza kwa ajili ya hali mbaya sana inayowajia.
2 Utajiri wenu umeoza, na mavazi yenu
yameliwa na nondo.
3 Dhahabu yenu na fedha yenu zimeliwa na
kutu. Kutu yake itashuhudia dhidi yenu, nayo
itaila miili yenu kama vile moto. Mmejiwekea
hazina kwa ajili ya siku za mwisho.
4 Angalieni! Ule ujira wa vibarua waliolima
mashamba yenu mliouzuia kwa hila unapiga
kelele dhidi yenu, na vilio vya wavunaji vimefika
masikioni mwa Mwenyezi Mungu, Mungu wa
majeshi ya mbinguni.

5 Mmeishi duniani kwa anasa na kwa starehe;
mmejinenepesha tayari kwa siku ya kuchinjwa.
6 Mmewahukumu na kuwaua watu wenye
haki, waliokuwa hawapingani nanyi.

### *Uvumilivu katika mateso*

7 Kwa hiyo, ndugu zangu, vumilieni hadi kuja
kwake Bwana Isa. Tazameni jinsi mkulima angojavyo ardhi itoe mavuno yake yaliyo ya thamani, na jinsi anavyovumilia kwa ajili ya kupata mvua ya kwanza na ya mwisho.
8 Ninyi nanyi vumilieni, tena simameni imara,
kwa sababu kuja kwa Bwana Isa kumekaribia.
9 Ndugu zangu, msinung'unikiane, msije
mkahukumiwa. Hakimu amesimama mlangoni!
10 Ndugu zangu, waangalieni manabii walionena kwa jina la Mwenyezi Mungu, wakiwa mfano wa uvumilivu katika kukabiliana na mateso.
11 Kama mnavyojua, tunawahesabu wale
waliovumilia kuwa wabarikiwa. Mmesikia habari za uvumilivu wake Ayubu, na mmeona kile ambacho hatimaye Mwenyezi Mungu alimtendea. Mwenyezi Mungu ni mwingi wa huruma, na amejaa rehema.
12 Zaidi ya yote, ndugu zangu, msiape, iwe kwa
mbingu au kwa dunia, au kwa kitu kingine chochote. "Ndiyo" yenu na iwe ndiyo, na "Hapana" yenu iwe hapana, la sivyo mtahukumiwa.

### *Maombi ya imani*

13 Je, mtu yeyote miongoni mwenu amepatwa
na taabu? Basi inampasa aombe. Je, kuna

yeyote mwenye furaha? Basi na aimbe nyimbo za kusifu.

14 Je, kuna yeyote miongoni mwenu aliye mgonjwa? Basi inampasa awaite wazee wa kundi la waumini wamwombee na kumpaka mafuta kwa Jina la Bwana Isa.

15 Kule kuomba kwa imani kutamwokoa huyo mgonjwa, naye Bwana Isa atamwinua, na kama ametenda dhambi, atasamehewa.

16 Kwa hiyo, ungamianeni dhambi zenu ninyi kwa ninyi, na kuombeana ili mpate kuponywa. Maombi ya mwenye haki yana nguvu, tena yanafaa sana.

17 Ilya alikuwa mwanadamu kama sisi. Aliomba kwa bidii kwamba mvua isinyeshe, nayo haikunyesha juu ya nchi kwa muda wa miaka mitatu na miezi sita.

18 Kisha akaomba tena, nazo mbingu zikatoa mvua, nayo ardhi ikatoa mazao yake.

19 Ndugu zangu, yeyote miongoni mwenu akipotoka na kuicha kweli, naye akarejeshwa na mtu mwingine,

20 hamna budi kujua kwamba yeyote amrejeshaye mwenye dhambi kutoka upotovu wake, ataiokoa roho ya huyo mwenye dhambi kutoka mauti na kufunika wingi wa dhambi.

# Biblica® Toleo Wazi Neno: Maandiko Matakatifu

## The Holy Bible in Swahili: Open Neno: Maandiko Matakatifu 2024

copyright © 2018, 2024 Biblica, Inc.

Language: Kiswahili (Swahili)

Contributor: Biblica, Inc.

Biblica® Toleo Wazi Neno: Maandiko Matakatifu™ ONMM™
Hakimiliki © 2018, 2024 na Biblica, Inc.
Biblica® Open Kiswahili Contemporary Scriptures™
Copyright © 2018, 2024 by Biblica, Inc.

**Creative Commons License**

Kazi hii imewezeshwa kupitia idhini ya kundi la the Creative Commons Attribution-ShareAlike 4.0 International License (CC BY-SA). Ili kuona nakala ya idhini hii, angalia kwenye anwani tovuti ya http://creativecommons.org/licenses/by-sa/4.0 au uandike barua kwa Creative Commons, PO Box 1866, Mountain View, CA 94042, USA.

Biblica® ni alama ya biashara iliyosajilishwa na shirika la Biblica, Inc; unahitaji ruhusa ya kimaandiko kutoka kwa Biblica, Inc. ili kutumia alama ya biashara ya Biblica®. Kulingana na makubaliano ya leseni ya CC BY-SA, unaweza kutoa nakala na kusambaza kazi hii bila kuibadilisha kamwe, mradi tu udumishe alama ya biashara ya Biblica®. Ukibadilisha au kufasiri kazi hii, na hivyo ukanyambua kazi tofauti, sharti uondoe alama ya biashara ya Biblica®. Katika kazi uliyonyambua, sharti uarifu mabadiliko yako, na kutambua kazi yako hivi: "Kazi ya asili ya Biblica, Inc. inapatikana bila bei katika tovuti zawww.biblica.com na open.bible."

Ilani ya hakimiliki sharti iwe katika ukurasa wa kichwa au wa hakilimiliki kama ifuatavyo:

Biblica® Toleo Wazi Neno: Maandiko Matakatifu™ ONMM™
Hakimiliki © 2018, 2024 na Biblica, Inc.
Biblica® Open Kiswahili Contemporary Scriptures™
Copyright © 2018, 2024 by Biblica, Inc.

"Biblica" ni alama ya biashara iliyosajiliwa katika United States Patent and Trademark Office (ofisi ya hataza na alama za biashara Marekani) na shirika la Biblica, Inc. Imetumiwa na ruhusa.

"Biblica" is a trademark registered in the United States Patent and Trademark Office by Biblica, Inc. Used with permission.

Sharti pia uwasilishe kazi uliyonyambua kupitia kwa liseni hiyo hiyo ya CC BY-SA.

Ikiwa ungependa kujulisha Biblica, Inc. kuhusu tafsiri yako ya kazi hii, tafadhali wasiliana nasi katika tovuti https://open.bible/contact-us.

This work is made available under the Creative Commons Attribution-ShareAlike 4.0 International License (CC BY-SA). To view a copy of this license, visit http://creativecommons.org/licenses/by-sa/4.0 or send a letter to Creative Commons, PO Box 1866, Mountain View, CA 94042, USA.

Biblica® is a trademark registered by Biblica, Inc., and use of the Biblica® trademark requires the written permission of Biblica, Inc. Under the terms of the CC BY-SA license, you may copy and redistribute this unmodified work as long as you keep the Biblica® trademark intact. If you modify a copy or translate this work, thereby creating a derivative work, you must remove the Biblica® trademark. On the derivative work, you must indicate what changes you have made and attribute the work as follows: "The original work by Biblica, Inc. is available for free atwww.biblica.com and open.bible."

Notice of copyright must appear on the title or copyright page of the work as follows:

Biblica® Toleo Wazi Neno: Maandiko Matakatifu™ ONMM™

Hakimiliki © 2018, 2024 na Biblica, Inc.

Biblica® Open Kiswahili Contemporary Scriptures™

Copyright © 2018, 2024 by Biblica, Inc.

"Biblica" ni alama ya biashara iliyosajiliwa katika United States Patent and Trademark Office (ofisi ya hataza na alama za biashara Marekani) na shirika la Biblica, Inc. Imetumiwa na ruhusa.

"Biblica" is a trademark registered in the United States Patent and Trademark Office by Biblica, Inc. Used with permission.

You must also make your derivative work available under the same license (CC BY-SA).

If you would like to notify Biblica, Inc. regarding your translation of this work, please contact us at https://open.bible/contact-us.

This translation is made available to you under the terms of the Creative Commons Attribution Share-Alike license 4.0.

You have permission to share and redistribute this Bible translation in any format and to make reasonable revisions and adaptations of this translation, provided that:

You include the above copyright and source information.

If you make any changes to the text, you must indicate that you did so in a way that makes it clear that the original licensor is not necessarily endorsing your changes.

If you redistribute this text, you must distribute your contributions under the same license as the original.

Pictures included with Scriptures and other documents on this site are licensed just for use with those Scriptures and documents. For other uses, please contact the respective copyright owners.

Note that in addition to the rules above, revising and adapting God's Word involves a great responsibility to be true to God's Word. See Revelation 22:18-19.

2025-05-21

---

PDF generated using Haiola and XeLaTeX on 20 May 2025 from source files dated 21 May 2025

72687ba8-7233-577d-bf23-786df16f869d